JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3
Baruapepe: cg@dcea.go.tz
Tovuti: www.dcea.go.tz
Nukushi: 2152820

8Barabara ya
kivukoni,
S.L.P. 80327,
Dar es Salaam.

## TAARIFA KWA UMMA

### TANI 2.2 ZA DAWA ZA KULEVYA ZAKAMATWA TANGA NA DAR ES SALAAM.

**Dar es Salaam, Novemba 25, 2024.**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, imekamata jumla ya **kilogramu 2,207.56** za dawa za kulevya na dawa tiba zenye asili ya kulevya katika mikoa ya Tanga na Dar es Salaam. Watuhumiwa saba wanashikiliwa kuhusiana na dawa hizo.

Kati ya dawa zilizokamatwa, skanka ni **kilogramu 1,500.6**, methamphetamine **kilogramu 687.76**, heroin **kilogramu 19.20**, na **chupa 10** za dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Fentanyl.

Tarehe 14 Novemba, 2024, jijini Dar es Salaam, katika wilaya ya Kigamboni, mtaa wa Nyangwale, watuhumiwa **Mohamed Suleiman Bakar (40)** na **Sullesh Said Mhailoh (36)**, wote wakazi wa Mabibo, Dar es Salaam, walikamatwa wakiwa na **kilogramu 1,350.4** za dawa za kulevya aina ya skanka. Dawa hizo zilikuwa zimefichwa ndani ya nyumba aliyopanga mtuhumiwa Mohamed, ambayo aliitumia kama ghala la kuhifadhi dawa hizo. Aidha, dawa nyingine zilipatikana ndani ya gari aina ya **Nissan Juke** yenye namba za usajili **T 534 EJC**, zikiwa tayari kwa kusambazwa.

Tarehe hiyo hiyo, katika mtaa wa Pweza Sinza E, wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, mtuhumiwa **Iddy Mohamed Iddy (46),** mkazi wa Chanika Buyuni, alikamatwa akiwa na **kilogramu 150.2** za skanka, zilizokuwa zimefichwa katika maboksi ya sabuni na baadhi ya dawa hizo zikiwa zimefichwa kwenye boksi lililotengenezwa kwa bati ngumu na kupachikwa kwenye chassis ya gari aina ya Scania lenye namba za usajili wa Afrika Kusini **LN87XJGP**, ambalo limekuwa likitumika kusafirisha bidhaa mbalimbali kutoka nje ya nchi.

Vilevile, tarehe 17 Novemba, 2024, katika jiji la Tanga, watuhumiwa **Ally Kassim Ally (52)** na **Fahadi Ally Kassim (36)** walikamatwa mtaa wa Mwakibila wakiwa na kilogramu **706.96** za dawa aina ya heroin na methamphetamine. Baadhi ya dawa hizo zilipatikana ndani ya gari aina ya **Toyota Noah** yenye namba za usajili **T 714 EGX**, huku nyingine zikibainika kufichwa kwenye nyumba aliyopanga mtuhumiwa.

Tarehe 19 Novemba, 2024, katika mtaa wa Kipata na Nyamwezi Kariakoo jijini Dar es Salaam, watuhumiwa **Michael Dona Mziwanda (28)** mkazi wa Tabata Segerea, na **Tumpale Benard Mwasakila (32)** mkazi wa Temeke Mikoroshini, walikamatwa wakiwa na chupa kumi za dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Fentanyl wakiwa nazo katika duka la M-PESA. Aidha, katika operesheni hizi zilizofanyika, jumla ya magari matatu na boti moja vilivyohusika katika uhalifu huo vinashikiliwa.

Dawa zilizokamatwa ni nyingi na zingeweza kuwa na madhara makubwa kwa jamii na taifa ikiwa zingeingia mitaani. Dawa hizi haziathiri tu wale waliokwisha anza matumizi ya dawa za kulevya, bali pia wafanyabiashara hawa hulenga watu wengine ambao hawajaanza matumizi ili kutanua masoko yao. Walengwa wapya wanaweza kuwa mtu yeyote katika jamii au familia za Kitanzania. Hivyo, ni dhahiri kuwa jamii nzima inakabiliwa na hatari ya dawa za kulevya.

Kadhalika, Mamlaka imebaini kuwa wahusika wa biashara haramu ya dawa za kulevya hutumia mbinu ya kupanga nyumba ambazo zinageuzwa kuwa maghala ya kuhifadhi dawa za kulevya, huku wao wakiishi katika maeneo mengine.

Mamlaka inatoa rai kwa wamiliki wa nyumba kuwa makini wanapopangisha nyumba zao, kwani nyumba inayotumika kwa shughuli za dawa za kulevya ni kinyume cha sheria na inaweza kutaifishwa. Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95, imeweka katazo kwa mmiliki au msimamizi wa nyumba, msimamizi wa eneo au chombo cha usafirishaji kuruhusu vitumike kwa lengo la kutengeneza, kuvuta, kujidunga, kuuza au kununua dawa za kulevya.

Aidha, mmiliki anapojua kuwa kosa linatendeka kwenye eneo lake, anajukumu la kutoa taarifa kwa Mamlaka. Kushindwa kufanya hivyo ni kosa la jinai, na akitiwa hatiani, adhabu yake inaweza kuwa faini kuanzia shilingi milioni tano hadi milioni hamsini, au kifungo cha miaka mitano hadi miaka thelathini jela, au vyote kwa pamoja.

Mamlakaya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inatoa shukrani kwa wananchi wanaotoa ushirikiano kwa kuwafichua watu wanaojihusisha na dawa za kulevya na tunawahimiza wananchi wote kuendelea kutoa taarifa pale wanapobaini matukio yanayohusiana na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Imetolewa na,

Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA.**